

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITA

HALMASHAURI YA MJI GEITA S.L.P 384, GEITA



TANGAZO LA KAZI YA UZOAJI TAKA NGUMU NA UKUSANYAJI WA ADA ZA USAFI KATIKA KATA SABA MJINI GEITA NA USAFI KATIKA JENGO LA UTAWALA (MAGOGO) HALMASHAURI YA MJI GEITA

Tarehe 12/04/2021.

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Geita anapenda kuwatangazia wananchi wote wa Mkoa wa Geita kazi ya uzoaji wa taka ngumu na ukusanyaji wa ada za usafi katika kata saba zenye jumla ya mitaa 31 inayopata huduma ya uzoaji wa taka ngumu. Kata hizo ni Nyankumbu (Mitaa 4), Kalangalala (mitaa 11), Mtakuja (mitaa 3), Buhalahala (mitaa 4), Bombambili (Mitaa 2), Kanyala(mitaa 2) na Kasamwa (Mitaa 5) pamoja na Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji (Magogo)
2. Zabuni hii inalenga maeneo makuu matano ambayo ni kama yafuatayo :-
 - Ukusanyaji, usafirishaji na utupaji wa taka ngumu kutoka kwenye makazi, maeneo ya biashara na maeneo mengine ndani ya mitaa.
 - Kusafisha / kufagia maeneo ya wazi, mitaro na barabara
 - Kufyeka nyasi katika maeneo mbalimbali
 - Kufanya usafi kila mwisho wa mwezi.
 - Kukusanya ada ya usafi ya kila mwezi kulingana na viwango vilivyopo kwenye sheria ndogo ya usafi wa mazingira ya H/ Mji Toleo namba 629 ya mwaka 2018
3. Ili kuwa na vigezo vyta kupata kazi hii pamoja na masharti mengine, ni lazima waombaji wazingatia mambo yafuatayo :-
 - Kikundi /Kampuni/ shirika litakaloomba ni vyema litoke katika maeneo husika ili kurahisisha utendaji
 - Kikundi/kampuni/shirika lazima lihusishe mabalizi wa maeneo yao ili kurahisisha zoezi la uzoaji wa taka na ukusanyaji wa ada
 - Kikundi/kampuni/ shirika litatakiwa kuambatanisha mpango kazi wa jinsi kazi ya uzoaji wa taka itakavyokuwa inafanyika pamoja na ile ya ukusanyaji wa ada
 - Kikundi/kampuni/ shirika litatakiwa kuwa na vitende kazi vya kufanya usafi (Mifagio,vifaa kinga kama buti, overall , mask, gloves n.k, vifaa vya kuzolea na kusafirisha taka mfano maguta , mikokoteni n.k)
 - Kikundi/ kampuni/ shirika litatakiwa kuomba idadi ya mitaa ambayo wanaweza kuifanya kazi kwa ufanisi na isizidi mitaa 10 kwa kila kikundi/ shirika au kampuni moja
 - Kikundi/ shirika/ kampuni itatakiwa kuwa na uwezo wa kuwalipa vibarua wake kwa wakati bila kusubiria pesa za Halmashauri


- Kikundi/ shirika / kampuni itawajibika na kusimamiwa na ofisi za serikali za mitaa ya maeneo husika waliyo ombea kazi.
- Kikundi/ shirika/ kampuni inatakiwa iwe na uzoefu wa zabuni za usafi
- Kikundi/ shirika / kampuni inatakiwa iwe na ofisi ndani ya eneo ambalo wataombea kazi
- Kikundi/ shirika/ kampuni ikihitaji magari ya Halmashauri itakodi kwa gharama ambayo itakuwa kwenye makubaliano
- Kikundi/ shirika/kampuni itatakiwa kuwa na idadi ya watu wa kutosha kwa ajili ya kufanya usafi wa maeneo ya wazi na barabara
- Kikundi/kampuni/shirika litatakiwa kushiriki kwenye usafi wa mwisho wa mwezi ikiwemo kufanya usafi, ukaguzi na kuhamasisha jamii kufanya usafi kwenye mitaa yao na kutoa taarifa
- Kikundi kitatakiwa kuambatanisha cheti cha usajili wa kikundi na kampuni au shirika litatakiwa kuambatanisha leseni pamoja na cheti cha usajili wa kampuni

4. Utaratibu wa ukusanyaji wa ada na mgawanyo wa malipo utakuwa katika utaratibu ufuatao :

- Kikundi/kampuni/shirika litatumia mfumo wa serikali wa ukusanyaji wa mapato ambapo mashine maalum zitatumika kutolea risiti (POS)
- Kikundi/kampuni/shirika litabakiwa na 70% ya makusanyo na 30% itabaki Halmashauri
- Pesa za makusanyo zitaingizwa katika akaunti ya Halmashauri kila siku zinapokusanya na mwisho wa mwezi kikundi/shirika/kampuni kitapatiwa asilimia yake kutohana na makusanyo iliyokusanya
- Viwango vya kutoza ada vitatokana na viwango elekezi vilivyoko kwenye sheria ndogo ya usafi wa mazingira wa mji Toleo namba 629 ya mwaka 2018
- Kikundi/shirika/kampuni Italipa ada ya utupaji taka kwenye dampo la kisasa kama ilivyooneshwa kwenye sheria ndogo ya usafi nwa mji ya mwaka 2018.

5.Utaratibu wa usafishaji wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji (Magogo) utakuwa ndani na nje ya jengo

- 6 Maombi yote yawasilishwe katika Ofisi ya Kitengo cha Ugavi na Manunuzi Halmashauri ya Mji Geita iliyopo eneo la Magogo yakiwa yamefungwa kwa lakiri na anuani " **Katibu wa bodi ya zabuni Halmashauri ya mji S.L.P 384** siku za kazi yaani jumatatu hadi ijumaa muda wa saa 1: 30 asubuhi hadi saa 9: 30 Alasiri. kabla ya tarehe **21/04/2021** saa **4:00 asubuhi**. Ufunguzi wa zabuni hiyo utafanyika tarehe **21/04/2021** saa **4: 30 asubuhi**.



Eng. Felix Nlilio

Mkurugenzi

Halmashauri ya Mji

Geita

